MAPENDEKEZO YA TUME YA RIPOTI YA UTAFITI WA KISHERIA WA

ENEO LA USIMAMIZI WA UFAMASIA

INAWASILISHWA KWA MHESHIMIWA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA

JANUARI, 2023

SURA YA SABA

MAPENDEKEZO YA TUME NA HITIMISHO

Utangulizi

Sura hii imejielekeza katika kutoa mapendekezo ya Tume kutokana na yaliyojitokeza katika utafiti huu. Mapendekezo haya ni majumuisho ya matokeo ya ukusanyaji wa taarifa na maelezo kwa maeneo yaliyotumika kufanyiwa utafiti huu, kwa kuangalia sheria na uzoefu wa nchi mbali mbali, mashirika ya kimataifa, sera na sheria zinazohusiana na utafiti huu, pamoja na maoni tofauti ya wadau. Tume baada ya kufanya utafiti huo, Inakuja na mapendekezo kama ifuatavyo:

Mapendekezo ya Kisera

Tume inapendekeza Sera iliyopo ifanyiwe mapitio kwa kujumuisha maeneo muhimu ya kuwasimamia na kuwadhibiti wataalam wa dawa. Maeneo ya jumla ambayo inapendekezwa Sera izingatie ni pamoja na:

Miongozo Kuhusu Taaluma ya Wataalam wa Dawa

Tume inapendekeza kuwa, katika kuzingatia umuhimu wa kipekee wa kada hii ya ufamasia, msiingi mizuri ya kitaaluma inahitajika kuwekwa kwenye Sera, kwa ajili ya kuwatambua wafamasia na usimamizi wa taaluma ya ufamasia, pamopja na kuweka uhusiano wa kada hii na ubora wa vyuo na taasisi za elimu ya ufamasia na ubora wa wakufunzi wenyewe.

Mikakati ya Usimamizi na Udhibiti wa Wataalam wa Dawa

Kulingana na wingi wa idadi ya wataalam wa dawa nchini, wakiwemo wafamasia, wimbi la biashara ya dawa limekua sana. Hivyo, Tume inapendekeza Sera ya dawa kutambua na kuanisha mikakati ya msingi ya kuwasimamia na kuwaratibu wafamasia.

Ushirikiano wa Taasisi Mbali Mbali

Kada ya ufamasia inafungamana na taasisi mbali mbali zikiweo zinazohusiana na fani ya ufamasia kama taasisi zinazotumia wafamasia na vyuo vya ufamasia. Hivyo, Tume inapendekeza kuwa Sera itambue haja ya ushirikiano na taasisi za muungano zikiwemo taasisi za kielimu kama NACTE, TCU na taasisi nyenginezo. Aidha, Tume inapendekeza kuwa chombo cha usimamizi wa wafamasia Zanzibar kiwe na ushirikiano na taasisi nyengine zisizo za kitaaluma ambazo kwa namna moja au nyengine zinafanya kazi na zina umuhimu kwa tasnia ya ufamasia na usimamizi wake kwa ujumla.

Mikakati ya Usimamizi wa Chombo cha Wataalam wa Dawa

Sera ya dawa imetambua umuhimu wa uanzishwaji wa mabaraza ya kitaalamu, ambayo inatumika katika kuwadhibiti na kuwasimamia wataalam wa dawa, wakiwemo wafamasia. Hivyo, Tume inapendekeza kuwa Sera hiyo ianishe na kutambua vyombo hivyo vinavyowahudumia na kuwasaidia wananchi likiwemo Baraza la Usimamizi wa wafamasia.

Mapendekezo ya kisheria

Kuanzishwa sheria maalum ya kusimamia Wafamasia

Tume inapendekeza kuanzishwa sheria maalum itakayosimamia wafamasia, wafamasia wasaidizi, wafamasia wa muda na wafamasia wa kigeni ili kuratibu vizuri shughuli za ufamasia, vigezo vya utendaji kitaalamu, huduma na vifaa kwa kazi za ufamasia.

Aidha, Tume inapendekeza sheria hiyo izingatie maeneo yafuatayo:

Vifungu vya jumla vitakavyozingatia misingi ya sheria, mamlaka ya sheria, na vifungu vyengine vya utangulizi;

Uanzishwaji wa chombo maalum cha usimamizi;

Usimamizi na udhibiti wa wafamasia;

Usajili wa wafamasia na maeneo ya kufanyia shughuli za ufamasia;

Masuala ya usajili, leseni na taratibu zake;

Utendajikazi wa kada ya ufamasia na wafamasia ambayo itatambua wafamasia kwa Zanzibar, sifa za wafamasia, usimamizi na majukumu ya wafamasia, maadili ya wafamasia, masharti ya utaalamu kwa wafamasia;

Viwango vya utendaji na huduma za ufamasia ambavyo vitajumuisha masharti na vigezo kwa maeneo ya kufanyiakazi wafamasia, utekelezaji na usimamizi;

Masuala ya nidhamu na taratibu zake;

Ukaguzi na masharti ya ukaguzi;

Makosa na Adhabu;

Kuanzishwa miongozo na kanuni katika kada ya wafamasia.

Kuundwa Baraza la Wafamasia

Tume inapendekeza kuwekwa kwa masharti ya kisheria ya kuanzishwa Baraza la Wafamasia ambalo litajumuisha muundo wa Baraza, uwezo, uundaji wa kamati ndogo ndogo ambazo zitasaidia kusimamia shughuli na uendeshaji wa wafamasia, kazi za Baraza, taratibu za uteuzi wa wajumbe wa Baraza, sifa na muda wa wajumbe wa Baraza. Aidha inapendekezwa majukumu ya Baraza la Ufamasia yajumuishe:

kuamua masuala yanayohusiana na usajili wa wafamasia na maduka ya wafamasia;

kuhakikisha usimamizi wa viwango vya juu vya utendaji na mwenendo wa wafamasia;

kuweka viwango vya elimu na mafunzo ya wafamasia;

kuamua masuala yanayohusiana na uteuzi na usajili wa watu kama wauzaji walioidhinishwa, kwa mujibu wa sheria;

kudhibiti na kuweka viwango vya maadili kwa wafamasia, mafundi sanifu wa dawa na wasaidizi wa dawa;

kutathmini sifa za kitaaluma na kiutendaji za wafamasia;

kuidhinisha taasisi na mitaala ya mafunzo ya kada ya wafamasia, na wasaidizi wa dawa;

kuhimiza utafiti katika somo la ufamasia ili kupata ustawi na maendeleo ya taaluma ya ufamasia;

kuelimisha umma juu ya masuala ya ufamasia na matumizi sahihi ya famasi na dawa;

kutoa ushauri Serikalini kwa lengo kuendeleza kada ya wafamasia;

Aidha, Tume inapendekeza Muundo wa Baraza la Ufamasia ujumuishe wataalam wenye kada tofauti zitakazoweza kusaidia Baraza kufanya kazi kwa ufanisi, na mahsusi inapendekezwa Baraza lijumuishe:

Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais, ambaye atakuwa mtu mwenye utaalamu na uzoefu usiopungua miaka tisa katika fani ya ufamasia au fani nyengine zinazofanana;

Mfamasia Mkuu wa Serikali ambaye atakuwa Katibu wa Baraza;

Wafamasia wawili waliosajiliwa kutoka sekta binafsi, wenye uzoefu usiopungua miaka saba watakaoteuliwa na Wazir anayehusika na masuala ya afya;

Mfamasia kutoka Wizara ya afya;

Mkurugenzi wa Bohari ya Dawa

Mwakilishi wa sekta ya elimu ya juu yenye mnasaba na sekta ya afya atakayeteuliwa na Waziri anayehusika na masuala ya afya;

Mkurugenzi anayehusika na masuala ya Tiba;

Mjumbe kutoka Chama cha Wafamasia;

Mkemia Mkuu wa Serikali;

Mwanasheria kutoka Wizara inayohusiana na masuala ya afya ambaye atakuwa Katibu wa Baraza;

Afisa mwandamizi anayehusika na udhibiti wa Dawa za Kulevya kutoka Mamlaka ya Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar.

Usajili wa wafamasia

Tume inapendekeza kuwekwa masharti ya usajili wa wafamasia kwa kuzingatia:

sifa na uteuzi wa Msajili;

Usajili wa wafamasia na taratibu za maombi ya usajili, malipo ya ada, uwepo wa daftari la usajili ambalo litaweka taarifa ya wafamasia waliosajiliwa na sifa zao;

Uwezo au mamlaka ya kukataa usajili kwa mujibu wa vigezo vya kisheria;

Utaratibu wa kutoa hati za usajili kwa wafamasia;

usajili wa muda na masharti yake

Kufutwa kwa usajili;

kuweka masharti maalum kwa mujibu wa kada za ufamasia

Kurekebisha daftari la usajili na kuweka sawa taarifa;

Tume inapendekeza Msajili wa Wafamasia awe mzanzibari na angalau mwenye shahada ya kwanza ya ufamasia; awe amesajiliwa kufanya kazi za ufamasia Zanzibar; awe na uzoefu wa kufanya kazi ya Ufamasia kwa kipindi kisichopungua miaka 15 na sifa za Uongozi na awe ni mwajiriwa wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Usajili wa majengo

Tume inapendekeza sheria iweke masharti ya usajili wa majengo na maduka ya dawa kwa kuzingatia:

Usajili wa majengo kama duka la dawa kwa kuzingaia sheria;

Ada au malipo ya usajili;

Utoaji wa hati ya usajili;

Daftari maalum la Maduka ya Dawa, anwani na maelezo ya majengo na pahala;

Muda wa kuomba tena leseni au usajili;

Kufuta usajili au kusimamisha biashara;

Masharti ya kubadilisha eneo la biashara;

Masharti ya uhifadhi kwa ajili ya kuuza au kuuzwa na maeneo salama ya kuhifadhia dawa;

Vigezo na Masharti katika maduka ya dawa ikiwemo kigezo cha duka la dawa kufunguliwa na mfamasia.

Masharti ya kuuza dawa

Inapendekezwa kuwekwa masharti ya kuuza dawa katika maduka na maeneo yanayoruhusiwa katika sheria, kwa kuzingatia:

Sifa za watu wanaotakiwa kuuza dawa;

Uuzaji wa jumla au rejareja chini ya udhibiti au usimamizi wa mfamasia;

usambazaji au uuzaji wa dawa na taratibu pamoja na watu wanaoruhusiwa kufanya kazi hiyo kama:

mfamasia aliyesajiliwa, au

daktari, daktari wa meno au daktari wa mifugo aliyesajiliwa kwa mujibu wa masharti ya Madaktari, au

mfamasia au mtu aliyeidhinishwa chini ya Sheria ya Wafamasia;

sharti la kuthibitisha mahitaji yaliyoainishwa kabla ya kutoa dawa;

Usajili wa famasi;

Vigezo vya famasi na utaratibu wa hati za usajili.

Chombo cha Kusimamia Masuala ya Kinidhamu

Tume inapendekeza kuwekwa chombo maalum cha kushughulikia masuala ya kinidhamu kwa wafamasia ili kuhakikisha maadili yanafuatwa. Inapendekezwa makosa ya maadili yajumuishe:

Ukiukaji wa kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria;

Kutoa dawa bila agizo la daktari;

kutolipa ada ya usajili ya kila mwaka kwa tarehe iliyowekwa;

Ubadilishaji wa maagizo bila idhini/ridhaa ya Daktari aliyesajiliwa;

Kuruhusu cheti chake cha usajili kutumika kinyume na utaratibu;

Kutotunza na kuweka kumbukumbu kama inavyotakiwa;

Kuzuia kwa makusudi mkaguzi au afisa aliyeteuliwa;

Kukiuka maadili ya kazi yake au maadili ya kiutumishi kinyume na Sheria hii au sheria nyengine zinazohusiana na maadili;

kutumia vibaya taaluma yake;

kutiwa hatiani kwa makosa ya jinai yanayoathiri utendaji;

kupotosha taarifa;

kufanya uzembe katika utekelezaji wa majukumu yake, kunakoweza kupelekea madhara kwa mtumiaji wa dawa.

Aidha, Tume inapendekeza adhabu za makosa ya maadili zijumuishe:

hatua dhidi ya mfamasia;

kutoa onyo au karipio;

kusimamisha usajili wake kwa muda maalum;

kufuta usajili;

kuondoa jina la mafamsia katika Daftari la Usajili;

kufikisha mahakamani

kulipa fidia

kurudisha kwa Msajili cheti cha usajili.

Kutoa haki ya Rufaa

Tume inapendekeza sheria itoe haki ya rufaa kwa mfamasia ambaye hatoridhika na maamuzi ya Baraza, na hivyo kumpa nafasi ya kukata rufaa katika ngazi mbali mbali ikiwemo ngazi ya Mahkama.

Masharti ya kutoa dawa kwa wafamasia

Tume inapendekeza kwamba sheria iweke masharti ya kutoa dawa kwa wafamasia ambayo yatazingatia:

Mfamasia kutotoa dawa bila ya agizo la daktari au maelekezo kutoka kwa daktari, daktari wa meno au daktari wa mifugo

Kila mfamasia ataweka na kutunza kumbukumbu za dawa yoyote iliyoelekezwa na daktari na dawa hizo zitatolewa kupitia fomu ya kumbukumbu iliyotolewa na Baraza kwa ajili hiyo.

Kujifananisha na kufanya kazi za ufamasia

Tume inapendekeza sheria ikataze mtu kufanya kazi ya ufamasia bila kuidhinishwa au kutumia majina ya wataalamu kinyume na sheria kwa nafasi za:

mfamasia;

daktari wa dawa;

mfamasia mwenye mamlaka ya kuchanganya au kutayarisha dawa;

mkemia wa dawa;

mtoaji wa dawa;

Aidha inapendekezwa sheria ibainishe marufuku, isipokuwa kwa mfamasia aliyesajiliwa, kuweka au kuonesha ishara, nembo au uwakilishi unaojumuisha maneno "duka la kuuza dawa","zahanati", au "duka la dawa", au ishara

nyengine yoyote, nembo au uwakilishi unaomaanisha au kuufanya umma kudhani kuwa majengo hayo yamesajiliwa kama maduka ya dawa.

Wakaguzi wa Wafamasia

Tume inapendekeza kutambuliwa wakaguzi wa wafamasia, kazi, uwezo, masharti na mamlaka yao, pamoja na kuweka vifungu vitakavyozungumzia:

Idadi ya wakaguzi inayohitajika kwa kila eneo

Maeneo ya kufanyia ukaguzi kama usajili, shughuli zinazoendeshwa, bidhaa za dawa, majengo ya daktari, daktari wa meno au upasuaji wa mifugo, au majengo mengine yoyote na kadhalika.

Kujiridhisha iwapo masharti ya sheria yanazingatiwa

kuchukua sampuli kama inahitajika ili kuhakikisha kama Sheria hii inafuatwa.

kuchunguza vitabu na taarifa mbalimbali

maeneo ya uhifadhi

fomu zote za kumbukumbu zinazohitajika kuwekwa

Aidha, Tume inapendekeza kuainishwa majukumu ya wafamasia na wafanyakazi wakati wa ukaguzi ikiwemo:

kutoa ushirikiano kwa mkaguzi anayeingia kwenye eneo

msaada au taarifa ndani ya uwezo wake kama itakavyohitajika.

Sifa za wafamasia na wasaidizi

Tume inapendekeza sheria ibainishe sifa za wafamasia na wasaidizi na kuweka masharti ya utendaji kazi kitaaluma kwa kutumia viwango vya:

Kufanya kazi kwa uweledi;

uhusiano wa kikazi na wagonjwa wao;
kuzingatia taarifa zinazofaa kwa kila mgonjwa;
Kuzingatia maelezo ya mgonjwa na kushauri au kumuelekeza kitaalamu inapobidi;
Kutoa dawa kwa mujibu wa maelekezo.

Tathmini na uwezo wa wafamasia

Tume inapendekeza kuwekwa utaratibu wa kufanya tathmini kwa wafamasia na wasaidizi ili kupima utendaji na kujua mapungufu yaliyopo katika kada hii. Aidha, tathmini hiyo izingatie utendaji wa kazi na utekelezaji wa majukumu ya msingi ya wafamasia, na maeneo ya kufanyia kazi na biashara kwa wafamasia ikilinganishwa na misingi ya maadili iliyopo.

Inapendekezwa kuwekwe vifungu vya kufanyia tathmini vigezo vya kitaaluma kwa ajili ya usajili wa wafamasia, uwezo unaolingana na taaluma na uwezo wa kisayansi unaohitajika.

Kuwekwa masharti ya elimu na kuendeleza wafamasia

Tume inapendekeza kuwekwa masharti ya kuendeleza wafamasia kupitia utaratibu wa utoaji wa elimu na mafunzo kwa wafamasia wakiwa kazini, mafunzo ya kujiendeleza wafamasia, usimamizi wa mafunzo na taratibu za tathmini na mtihani wa majaribio juu ya uwezo wa kitaaluma.

Utaratibu wa mafunzo kwa vitendo (internship)

Inapendekezwa sheria itambue na iweke utaratibu wa mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi wanaomaliza masomo ya ufamasia, muda wa mafunzo

utakaotambuliwa, kutambuliwa mazoezi ya vitendo, wasimamizi wa mafunzo na taratibu za tathmini na sifa za kusajiliwa katika mafunzo.

Dhima ya Kushtakiwa

Tume pia inapendekeza sheria itakayotungwa iweke kifungu cha kuwalinda watendaji wa Baraza la ufamasia dhidi ya mashauri yoyote kwa kitendo chochote kitakachokwenda kinyume na kazi za Baraza, ikiwa amefanya ndani ya majukumu ya kazi na wakati wa kutenda kitendo hicho alikuwa na nia nzuri. Inapendekezwa mashauri hayo badala yake yaelekezwe kwa uongozi wa Baraza la Ufamasia na yaeleze mtu ambae atakuwa na wajibu wa kujibu madai yoyote.

Kuwepo chama cha wafamasia kisheria

Tume inapendekeza sheria ikitambue Chama cha wafamasia kitakachokuwa na nguvu ya kusaidia usimamizi na udhibiti wa wafamasia ambacho kitaisaidia majukumu yaliyoainishwa kwa mujibu wa sheria hii kutekelezeka kwa ufanisi. Inashauriwa Sheria iweke masharti ya kuanzishwa kwa chama cha wafamasia ambacho kitasaidia kudhibiti na kusimamia kada ya ufamasia kwa baadhi ya majukumu ya msingi ya kada ya ufamasia ambapo shughuli zao zitasimamiwa na baraza la ufamasia.

Aidha, inapendekezwa kuwa moja katika masharti ya msingi ya kusajiliwa kwa mfamasia, iwe ni baada ya kukubaliwa na chama hicho cha wafamasia kuwa ana sifa za kuwa mfamasia. Hivyo, Baraza la Wafamasia halitokubali kumsajili mtu kuwa mfamasia mpaka litakapopata maoni ya chama cha wafamasia kuwa mtu huyo anafaa kuwa mfamasia. Chama hicho cha wafamasia kinaweza

kuweka utaratibu wa vigezo vya namna ya kuwapima na kuwapendekeza watu kuwa wafamasia.

Kufanyike Marekebisho ya Sheria No. 2 ya 2006

Kutokana na mapendekezo ya kutungwa kwa sheria mpya kama ilivyopendekezwa katika Sura hii, Tume inapendekeza kufanyiwa marekebisho Sheria ya Chakula, Dawa, na Vipodozi Nam. 2 ya mwaka 2006, ili kuondoa vifungu vinavyosimamia masuala ya ufamasia. Vifungu ambavyo vitahusika ni pamoja na:

Sehemu ya Pili ya Sheria katika sehemu ya usimamizi, kifungu cha 3, 4, 5, 6 vinapendekezwa virekebishwe ili kutenganisha mamlaka ya Baraza la Wafamasia na Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi.

Kurekebishwa kifungu cha 12 kinachohusiana na Kamati ya kitaalamu

Kurekebishwa kifungu cha 15 kinachohusu udhibiti na uingizwaji na utoaji wa dawa na masuala mengine;

Kifungu cha 16 na 17 kuhusu usajili wa maeneo ya biashara kama maduka ya dawa ili masharti yake yazingatiwe katika sheria mpya;

Kifungu cha 18-25 kuhusu utoaji wa vibali na taratibu kwa wafamasia vifutwe ili masharti hayo yazingatiwe katika Sheria inayopendekezwa kutungwa;

Sehemu ya 4, inayohusu wafamasia (kifungu 46-50) ifutwe ili izingatiwe katika Sheria inayopendekezwa kutungwa;

Vifungu vya 74-77 vinavyoohusu dawa zenye sumu au zinazohitaji matumizi maalum na udhibiti wake vizingatiwe tena.

Miongozo na kanuni

Mbali ya marekebisho ya Sheria yaliyoelezwa, inapendekezwa kuanzishwa miongozo na kanuni mbalimbali zikijumuisha Kanuni ya:

utendaji na kufanya kazi za ufamasia;

maadili;

Usajili wa wafamasia;

Usajili wa wafamasia wageni;

Ukaguzi na uchunguzi;

Elimu na mafunzo;

Elimu ya vitendo kwa wanafunzi;

Udhibiti na usimamizi;

Masuala ya maadili kwa wafamasia.

Mapendekezo ya kiutendaji

Pamoja na kuwepo kwa mambo mengi kuhusu sera na sheria, Tume inapendekeza mambo yafuatayo yawekewe utaratibu wa kiutendaji ili kuimarisha ufanisi Serikalini.

Serikali kuweka mifumo maalum ya kusimamia mafunzo ya taaluma na uwezo unaohitajika kutolewa katika taasisi za elimu Zanzibar, ili kutoa huduma bora na kudhibiti uwiano wa idadi ya wafamasia kutokuwa kubwa sana na kuepusha upungufu wa wafamasia, ili kufikia kiwango cha juu cha huduma za ufamasia katika sekta za Umma na Sekta binafsi.

Kuwekwe mipango mkakati ya mara kwa mara ili kulinda tasnia ya ufamasia, kwa wafamasia kufanya kazi kwa maadili na kutumia uweledi wao kwa lengo la ufanisi wa kuisaidia jamii kupambana na maradhi na kuwa na afya ya jamii bora, badala ya kujielekeza katika faida ya biashara ya dawa.

Hitimisho

Kada ya wafamasia na watu wanaohusika na shughuli za ufamasia ni eneo ambalo limekuwa kwa kasi na linahitaji usimamizi maalum, kwa kuzingatia miongozo ya Shirika la Afya Ulimwenguni, Sera, Dira ya maendeleo ya 2050, Ilani ya CCM 2020-2025 na miongozo mengine iliyopo Zanzibar.

Eneo hili linahitaji kuwekewa usimamizi wa karibu hasa katika maeneo ya kuwatambua na kuwasajili wafamasia, Udhibiti wa wafamasia kupitia chombo maalum, tathmini ya wafamasia, uwezo wa kufanyakazi kwa wafamasia kitaalamu, masuala ya maadili na nidhamu, kuendelezwa wafamasia, kulinda afya na usalama wa umma.

Pamoja na umuhimu wa wafamasia katika jamii, bado usimamizi wa taaluma zao ni jambo la lazima kwa maeneo yote ya kielimu, utendajikazi na nidhamu kwa mujibu wa kada ya ufamasia.

Hivyo, Ripoti hii imependekeza kuanzishwa sheria maalum ya kusimamia kada hii, pamoja na kuweka taratibu na miongozo ya usajili, maadili, ukaguzi, tathmini, usimamizi, uendelezaji wataalamu, makosa na adhabu na kulinda wafamasia.

REJEA

Ahmad M, Durr-e-Shahwar , Madiha , Madni A, Usman M, Asghar W: Economical and clinical impact of pharmacists' participation in patient care. 15th International Pharmacy Conference and Exhibition. 2009, Lahore: Pakistan Pharmacists Association

A. M. Rafferty, 'Th e Seductions of History and the Nursing Diaspora', Health and History, 7:2 (2005), pp. 2–16 on p. 6. See also Volume 1 of this collection.

A. Crozier, 'Sensationalising Africa: British Medical Impressions of sub-Saharan Africa 1890-1939', Journal of Imperial and Commonwealth History, 35:3 (2007), pp. 393–415.

A. Crozier, Practising Colonial Medicine: The Colonial Medical Service in British East Africa (London: I. B. Tauris, 2007), pp. 29–30.

Anderson S: The state of the worlds pharmacy: a portrait of the pharmacy profession. Journal of Interprofessional Care. 2002, 16: 391-404

Ashcroft, R. E.; Dawson, A.; Draper, H & McMillan, J. R. (2007) Principles of Healthcare Ethics, 2nd edition (Chichester: John Wiley & Sons, Ltd

Auguste, V. Guerin, C & Hazebroucq, G. (1997) 'Opinions and practices with regard to confidentiality in French hospital pharmacies' The International Journal of Pharmacy Practice 5: 122-7

Annual Report 2020 - Pharmacy Council NZ https://pharmacycouncil.org.nz › uploads › 2021/03

Ahmadi K, Ahmad Hassali MA. Professionalism in pharmacy: a continual societal and intellectual challenge. Am J Pharm Educ. 2012;76:72

Broadbent J. If you can't measure it, how can you manage it?: management and governance in higher educational institutions. Public Money Manag. 2007;27:193–198

Briscoe-Dwyer L, Ethics and professional obligation *American Journal of Health-System Pharmacy* 2006 63(7):615-16

Beauchamp and Childress (2001) Principles of Biomedical Ethics (USA: Oxford University Press)

Bissell, P.; Anderson, C.; Savage, I.; Goodyear, L. (2001) 'Supplying emergency hormonal contraception through patient group direction: a qualitative study of the views of pharmacists' The International Journal of Pharmacy Practice 9: Supplement pR57

Crompton, G. K. (1979) 'Ethics of Drug Promotion' British Medical Journal Nov 3; 2 (6198):1141

Casper Andersen, Andrew Cohen (ed) Decree by His Highness Seyyid Ali Bin Hamoud, Sultan of Zanzibar. No. 4 of 1909. Public Health', in Zanzibar, Sultan's Decrees Issued during the Year 1909 (London: House of Lords, 1909) in the book THE GOVERNMENT AND ADMINISTRATION OF AFRICA, 1880–1939 Edited by Casper Andersen and Andrew Cohen Volume 5 Health, Labour and Other Issues of Administration First Published2013 Edition 1st Edition Routledge

Cribb and Barber (2000) Developing Pharmacy Values: Stimulating the Debate - A Discussion Paper (London: Royal Pharmaceutical Society of Great Britain)

Christine Venter, Jackie Maimin, Yahya Essop Choonara, Sarel Malan, Mosiuoa Shadrack Shuping, Pieter Kilian, Jan du Toit, Natalie Shellack, Josephine Herbert, Helen Hayes SOUTH AFRICAN PHARMACY COUNCIL SOUTH AFRICAN PHARMACY COUNCIL ANNUAL REPORT 2019 ANNUAL REPORT 2019

Code of Pharmacy Council on the Ethics of Pharmacy Profession, B.E. 2538. (21 December 1995). Government Gazette; 112(102 D): 63-7.

CPM (Center for Pharmaceutical Management). Access to essential medicines: Tanzania, 2001, Prepared for the Strategies for Enhancing Access to Medicines Program. Arlington, VA: Management Sciences for Health; 2003.

Delpasand K, Kiani M, Afshar L, NazariTavakkoli S, shirazi SF, Extracting the ethical challenges of pharmacy profession in Iran, a qualitative study *Journal of Research in Medical and Dental Science* 2018 6(1):10-15.

Davis, P. (1997). Managing Medicines: Public Policy and Therapeutic Drugs, Buckingham: Open University Press.

Denzin, N. K. (1968) 'Incomplete professionalization: the case of pharmacy' Social Forces 46; 3: 375-381

Deans Z, Ethics in pharmacy practice 2010 London Pharmacy Practice Research Trust

East and Central African Journal of Pharmaceutical Sciences Vol.14 (2011) 64-72 The role of pharmacists in diabetes management in Zanzibar and Dar es Salaam regions, Tanzania K.D. MWAMBETE1*,

Ecclestone, B. (1998). Careers in Pharmacy, London: The Pharmaceutical Press

Etemadian MN, *Medical ethics and customs* 1963 Tehran University Press

Gilbert L: To Diagnose, Prescribe and Dispense: Whose Right Is It? The Ongoing Struggle Between Pharmacy and Medicine in South Africa. Current Sociology. 2001, 49: 97-118

Ghaffar A, Kazi BM, Salman M: An Overview of the Health Care System in Pakistan. Journal of Public Health Medicine. 1999, 22: 38-42.

Gibson B. 'Pharmacists and tobacco: dollars before duty' CMAJ. 1990 Mar 15;142; 6: 621- 632

Guideline - Informing a National Board about where you practice https://www.pharmacyboard.gov.au › documents

Hervey TK, McHale JV, *Health law and the European Union* 2004 Cambridge University Press

K. Vongsathorn, '"First and Foremost the Evangelist"? Mission and Government Priorities for the Treatment of Leprosy in Uganda 1927–1948', Journal of Eastern African Studies, 6:3 (2012), pp. 544–60. 15. For sources on the issue of labour in relation to economic development in Africa, see D. Sunderland (ed.) Economic Development of Africa, 5 vols (London: Pickering & Chatto, 2011), vol. 5.

Kelley KA, Stanke LD, Rabi SM, Kuba SE, Janke KK. Cross-validation of an instrument for measuring professionalism behaviors. Am J Pharm Educ. 2011;75:179

Kiene T, *"The" Legal Protection of Traditional Knowledge in the Pharmaceutical Field: An Intercultural Problem on the International Agenda* 2009 WaxmannVerlag

Li H, Ding N, Zhang Y, Liu Y, Wen D. Assessing medical professionalism: a systematic review of instruments and their measurement properties. PLoS One. 2017;12:e0177321

Latif, D. A. & Berger, B. A. (1997) Moral reasoning in pharmacy students and community practitioners. Journal of Social and Administrative Pharmacy 14; 3: 166-179

Lunde, I. & Dukes, G. (Eds) (1989), The Role and Function of the Community and Hospital Pharmacist in the Health care Systems of Europe, WHO Collaborating Centre for Clinical Pharmacology and Drug Policy Science, The Netherlands: Groningen

M. Vaughan, Curing Their Ills: Colonial Power and African Illness (Cambridge: Polity Press, 1991), pp. 38–9.

McMahon, Thomas R "The Professional's Responsibility." Journal of the American Pharmaceutical Association NSi 2:1 (July, 1972), pp. 358-59.

Mak VS, Clark A, March G, Gilbert AL. The Australian pharmacist workforce: employment status, practice profile and job satisfaction. Aust Health Rev. 2013;37:127–130

Metta E, Haisma H, Kessy F, Hutter I, Bailey A. "We have become doctors for ourselves": motives for malaria self-care among adults in southeastern Tanzania. Malar J. 2014;13:249

M. Justin-Temu And L. Zungufya, Department of Pharmaceutical Microbiology, School of Pharmacy, Muhimbili University of Health Allied Sciences, P. O .Box 65013 Dar es Salaam, Tanzania 2Department of Pharmaceutics, School of Pharmacy, Muhimbili University of Health Allied Sciences,.

Miklich MA, Reed BN, Mattingly TJ 2nd, Haines ST. Beliefs and behaviors of professionally engaged pharmacists. J Am Pharm Assoc (2003) 2016;56:405–411.

Mossialos E, Courtin E, Naci H, Benrimoj S, Bouvy M, Farris K, Noyce P, Sketris I. From "retailers" to health care providers: transforming the role of community pharmacists in chronic disease management. Health Policy. 2015;119:628–639.

Moullin JC, Sabater-Hernandez D, Fernandez-Llimos F, Benrimoj SI. Defining professional pharmacy services in community pharmacy. Res Social Adm Pharm. 2013;9:989–995.

Naffs, N.J. (2001) 'Pharmaceutical care until the end: the role of pharmacists in euthanasia in The Netherlands' Pharmacy World Science 23; 4: 129-31

Nelson, V. (1988) 'Promotion and selling of unnecessary food supplements: quackery or ethical pharmacy practice?' American Pharmacy; 10: 34-6

Panton, R. & Chapman, S. eds. (1998), Medicines Management, London: BMJ Books. RPSGB (1997), Building the Future: A Strategy for a Twenty-first Century Pharmaceutical Service, London: Royal Pharmaceutical Society of Great Britain

Pande, S, Hiller, JE, Nkansah, N, Bero, L. The effect of pharmacist-provided non-dispensing services on patient outcomes, health service utilisation and costs in low- and middle-income countries. Cochrane Database Syst Rev. 2013;(2):CD010398

Poyongo, B.P.; Sangeda, R.Z. Pharmacists' Knowledge, Attitude and Practice Regarding the Dispensing of Antibiotics without Prescription in Tanzania: An Explorative Cross-Sectional Study. *Pharmacy* 2020, *8*, 238, Journal of Public Health Policy Vol. 33, Supplement 1. Universities in transition to improve public health: A Tanzanian case study (2012), pp. s110-s125 (16 pages)

Resnik DB, Ranelli PL, Resnik SP, The conflict between ethics and business in community pharmacy: what about patient counseling? *Journal of Business Ethics: JBE* 2000 28(2):179-86

Rodgers R, Dewsbury C, Lea A, *Law and ethics in pharmacy practice (Vol. 5)* 2010 Pharmaceutical Press

R. Johnson, 'Th e West African Medical Staff and the Administration of Imperial Tropical Medicine 1902–1914', Journal of Imperial and Commonwealth History, 38:3 (2010), pp. 419–39.

Rovers JP, Currie JD, Hagel HP, McDonough RP, Sobotka JL: A practical guide to pharmaceutical care. 2003, Washington, DC: American Pharmaceutical Association

Steinbock, B., Arras, J. D. & London, A. J. (2003) Ethical Issues in Modern Medicine (USA: McGraw Hill)

Sharon Youmans, Olipa Ngassapa and Mhina Chambuso, Clinical pharmacy to meet the health needs of Tanzanians: Education reform through partnership across continents (2008—2011)

T. J. Johnson and M. Caygill, 'The British Medical Association and its Overseas Branches: A Short History', Journal of Imperial and Commonwealth History, 1:3 (1973), pp. 303–39, on p. 312.

Valimba R, Liana J, Joshi MP, Rutta E, Embrey M, Bundala M, et al. Engaging the private sector to improve antimicrobial use in the community: experience from accredited drug dispensing outlets in Tanzania. J Pharm Policy Pract. 2014;7(1):11.

Veatch, Robert M. "Professional Prerogatives: Perspectives of an Ethicist." American Journal of Pharmaceutical Education 55:1 (Spring, 1991), pp. 74-78.

Wafula FN, Miriti EM, Goodman CA. Examining characteristics, knowledge and regulatory practices of specialized drug shops in Sub-Saharan Africa: a systematic review of the literature. BMC Health Serv Res. 2012;12:223

Wills, S.; Brown, D. & Astbury, S. (2002) 'A survey of ethical issues surrounding supply of information to members of the public by hospital pharmacy medicines information centres' Pharmacy World and Science

Worley MM, Schommer JC, Brown LM, Hadsall RS, Ranelli PL, Stratton TP, Uden DL: Pharmacists' and patients' roles in the pharmacist-patient relationship: Are pharmacists and patients reading from the same relationship script?. Research in Social and Administrative Pharmacy. 2007, 3: 47-69

World Health Organisation (1997). The Role of the Pharmacist in the Health Care System: Preparing the Future Pharmacist, WHO, Geneva. (WHO/Pharm/97/599).
WORLD HEALTH ORGANISATION (2000). Better Quality at Lower Prices, WHO, Geneva, Switzerland (Press Release WHO/26)

World Health Organisation (1988). The Role of the Pharmacist in the Health Care System: Report of a WHO Consultative Group, New Delhi, India, and Report of a WHO Meeting, Tokyo, Japan, (WHO/Pharm/94.596).

Zammit D: How to make ethical decisions. The Pharmaceutical Journal. 2003, 271: 468-